
# UTABIRI WA MVUA ZA *MSIMU*
# (NOVEMBA, 2025 – APRILI, 2026)




***Kielelezo 1. Mwelekeo wa Mvua za Msimu (Novemba, 2025 hadi Aprili, 2026).***


*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*
Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Chuo Kikuu cha Dodoma,
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, 1 Mtaa wa CIVE,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610: Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz


**(IMETHIBITISHWA – ISO 9001:2015, Huduma za Hali ya Hewa kwa Usafiri wa Anga)**

## Dondoo muhimu za mvua za *Msimu* (Novemba, 2025 – Aprili, 2026)

Taarifa hii inatoa uchambuzi wa mwenendo wa mifumo ya hali ya hewa na mwelekeo wa mvua za Msimu kwa maeneo yanayopata msimu mmoja wa mvua kwa mwaka (kanda ya magharibi, kati, nyanda za juu kusini magharibi, kusini mwa nchi, ukanda wa pwani ya kusini pamoja na maeneo yaliyopo kusini mwa Mkoa wa Morogoro) katika kipindi cha miezi ya Novemba, 2025 hadi Aprili, 2026. Ushauri na tahadhari umetolewa kwa wadau wa sekta mbalimbali wanaotumia taarifa za hali ya hewa katika utekelezaji wa majukumu yao kama vile kilimo na usalama wa chakula, mifugo na uvuvi, maliasili, wanyamapori na utalii, nishati na maji, ujenzi, usafiri na usafirishaji (nchi kavu, kwenye maji na angani), mamlaka za miji, afya, sekta binafsi pamoja na menejimenti za maafa. Muhtasari wa mwelekeo wa mvua hizo na athari zake ni kama ifuatavyo:

**a) Mwelekeo wa mvua za Msimu kwa maeneo yanayopata msimu mmoja wa mvua kwa mwaka:**

(i) Mvua za Chini ya Wastani hadi Wastani zinatarajiwa katika mikoa ya Kigoma, Tabora, Katavi, Singida na Dodoma. Aidha, mvua za Wastani hadi Chini ya Wastani zinatarajiwa katika mikoa ya Njombe, Iringa, Mbeya, Songwe, Rukwa, Ruvuma, Mtwara na Lindi pamoja na kusini mwa mkoa wa Morogoro. Msimu unatarajiwa kutawaliwa na vipindi virefu vya ukavu na mtawanyiko wa mvua usioridhisha katika maeneo mengi.

(ii) Mvua zinatarajiwa kuanza kati ya wiki ya tatu na ya nne ya mwezi Oktoba, 2025 katika mikoa ya Tabora, Katavi na Kigoma; na kusambaa katika mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Iringa, Njombe pamoja na kusini mwa mkoa wa Morogoro kati ya wiki ya pili na ya tatu ya mwezi Novemba, 2025. Mvua hizi zinatarajiwa kuisha kati ya wiki ya nne ya mwezi Aprili na wiki ya kwanza ya mwezi Mei 2026 katika maeneo mengi.

(iii) Kipindi cha nusu ya pili ya msimu (Februari – Aprili, 2026) kinatarajiwa kuwa na ongezeko la mvua ikilinganishwa na nusu ya kwanza (Novemba, 2025 – Januari, 2026).

**Athari na ushauri**

(i) Mvua za Chini ya Wastani zinazotarajiwa katika maeneo mengi zinaweza zikasababisha upungufu wa unyevu wa udongo, jambo ambalo linaweza kuathiri ukuaji na maendeleo ya mazao na kupunguza mavuno hususani kwa mazao yanayategemea mvua.

(ii) Kupungua kwa kina cha maji kwenye mabwawa na mtiririko wa maji kwenye mito kunaweza kutokea, hali ambayo inaweza kupunguza upatikanaji wa maji kwa matumizi mbalimbali.

(iii) Upatikanaji wa maji na malisho kwa ajili ya mifugo unatarajiwa kuathirika.

## 1. MWENENDO WA MVUA ZA VULI, 2025 NA MWELEKEO WA MVUA ZA MSIMU (NOVEMBA, 2025 HADI APRILI, 2026)

### 1.1 Mwenendo wa Mvua za Vuli (Oktoba-Disemba), 2025

Msimu wa mvua za Vuli kwa miezi ya Oktoba hadi Desemba, 2025 katika maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka (Mikoa ya Kagera, Geita, Mwanza, Shinyanga, Simiyu, Mara, Manyara, Arusha, Kilimanjaro, Tanga, Dar es Salaam, kaskazini mwa mkoa wa Morogoro, Pwani (ikijumuisha visiwa vya Mafia) pamoja na Zanzibar (visiwa vya Unguja na Pemba)) utabiri wake ulitolewa tarehe 11 Septemba, 2025. Mvua za Wastani hadi Chini ya Wastani zilitabiriwa katika maeneo mengi ya pwani ya kaskazini, nyanda za juu kaskazini mashariki, mikoa ya Mara, Simiyu, Mwanza na Shinyanga. Hata hivyo, mvua za Wastani hadi Juu ya Wastani zilitabiriwa katika maeneo ya mikoa ya Kagera, Geita na kaskazini mwa mkoa wa Kigoma.

Msimu wa mvua za *Vuli*, 2025 ulitarajiwa kutawaliwa na vipindi virefu vya ukavu na mtawanyiko wa mvua usioridhisha hususan katika maeneo ya pwani ya kaskazini na nyanda za juu kaskazini mashariki. Aidha, mvua hizo zilitarajiwa kuanza wiki ya kwanza na ya pili ya mwezi Oktoba, 2025 katika maeneo ya mikoa ya Kagera, Geita, Mwanza, Mara na kaskazini mwa mkoa wa Kigoma; na kusambaa katika maeneo ya pwani ya kaskazini na nyanda za juu kaskazini mashariki wiki ya kwanza na ya pili ya mwezi Novemba 2025. Mvua zilitabiriwa kuisha mwezi Januari, 2026.

Mvua hizo zimeanza katika baadhi ya maeneo ya ukanda wa Ziwa Victoria kama ilivyotabiriwa. Hata hivyo, maeneo ya pwani ya kaskazini na nyanda za juu kaskazini mashariki yameendelea kutawaliwa na vipindi virefu vya ukavu.

### 1.2 Mwelekeo wa mvua za Msimu (Novemba, 2025 hadi Aprili, 2026)

Mvua za Msimu ni mahususi katika maeneo ya magharibi mwa nchi (Mikoa ya Kigoma, Tabora na Katavi), kanda ya kati (mikoa ya Singida na Dodoma), nyanda za juu kusini magharibi (mikoa ya Njombe, Iringa, Mbeya, Songwe na Rukwa), kusini mwa nchi (mkoa wa Ruvuma), ukanda wa pwani ya kusini (mikoa ya Lindi na Mtwara) pamoja na maeneo ya kusini mwa mkoa wa Morogoro. Maeneo haya yanapata msimu mmoja wa mvua kwa mwaka, unaoanza mwezi Novemba na kuisha kati ya mwezi Aprili na Mei ya mwaka unaofuata.

Kutokana na mifumo ya hali ya hewa inayotarajiwa (kama inavyoelezwa katika kipengele cha 2 cha taarifa hii), mvua za Chini ya Wastani hadi Wastani zinatarajiwa katika mikoa ya Kigoma, Tabora, Katavi, Singida na Dodoma. Hata hivyo, mvua za Wastani hadi Chini ya Wastani zinatarajiwa katika mikoa ya Njombe, Iringa, Mbeya, Songwe, Rukwa, Ruvuma, Mtwara na Lindi pamoja na maeneo ya kusini mwa mkoa wa Morogoro.

Mvua za *Msimu* zinatarajiwa kuanza kati ya wiki ya tatu na ya nne ya mwezi Oktoba, 2025 katika mikoa ya Tabora, Katavi na Kigoma; na kusambaa katika mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Iringa, Njombe pamoja na kusini mwa mkoa wa Morogoro kati ya wiki ya pili na ya tatu ya mwezi Novemba, 2025. Mvua hizi zinatarajiwa kuisha kati ya wiki ya nne ya mwezi Aprili na wiki ya kwanza ya mwezi Mei 2026 katika maeneo mengi. Kwa ujumla, Msimu unatarajiwa kutawaliwa na vipindi virefu vya ukavu na mtawanyiko wa mvua usioridhisha katika maeneo mengi.

Ongezeko la mvua linatarajiwa katika kipindi cha nusu ya pili ya msimu (Februari – Aprili, 2026) ikilinganishwa na nusu ya kwanza (Novemba, 2025 – Januari, 2026). Maelezo ya kina juu ya mwelekeo wa mvua hizo za msimu ni kama ifuatavyo:

i. **Kanda ya Magharibi: (Mikoa ya Tabora, Katavi na Kigoma):**

Mvua za Chini ya Wastani hadi Wastani zinatarajiwa katika mikoa hii na zinatarajiwa kuanza wiki ya tatu na ya nne ya mwezi Oktoba, 2025 na kuisha wiki ya nne ya mwezi Aprili na wiki ya kwanza ya mwezi Mei, 2026.

ii. **Kanda ya Kati: (Mikoa ya Singida na Dodoma):**


Mvua katika maeneo haya zinatabiriwa kuwa za Chini ya Wastani hadi Wastani na zinatarajiwa kuanza wiki ya kwanza na ya pili ya mwezi Desemba, 2025 na kuisha wiki ya tatu na ya nne ya mwezi Aprili, 2026.

iii. **Nyanda za juu kusini magharibi (Mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Iringa, Njombe, pamoja na maeneo ya kusini mwa mkoa wa Morogoro):**

Mvua za Wastani hadi Chini ya Wastani zinatabiriwa katika maeneo haya. Mvua zinatarajiwa kuanza wiki ya pili na ya tatu ya mwezi Novemba, 2025 na kuisha wiki ya nne ya mwezi Aprili na wiki ya kwanza ya mwezi Mei, 2026.

iv. **Pwani ya kusini na maeneo ya kusini mwa nchi: (Mikoa ya Lindi, Mtwara na Ruvuma):**

Mvua zinatarajiwa kuwa za Wastani hadi Chini ya Wastani katika mikoa hii. Mvua zinatarajiwa kuanza wiki ya kwanza na ya pili ya mwezi Desemba, 2025. Mvua zinatarajiwa kuisha wiki ya nne ya mwezi Aprili na ya kwanza ya mwezi Mei, 2026.




**Kielelezo 2: Kushoto: Mwelekeo wa mvua za *Msimu* (Novemba, 2025–Aprili, 2026) na Kulia: Wastani wa muda mrefu (miaka 30) wa mvua za *Msimu* (1991-2020).**

***Angalizo 1:*** *Izingatiwe kuwa matukio ya vipindi vya mvua kubwa yanaweza kujitokeza hata katika maeneo yanayotarajiwa kupata mvua za chini ya wastani.*

***Angalizo 2:*** *Mwelekeo wa mvua uliotolewa hapa umezingatia zaidi kipindi cha mvua za Msimu (miezi sita) na hali ya mvua katika maeneo makubwa. Hivyo, viashiria vinavyochangia mwenendo wa mifumo ya mvua na mabadiliko ya muda mfupi vitazingatiwa katika utabiri wa kila siku na utabiri wa kila mwezi. Watumiaji wa taarifa hii wanashauriwa kufuatilia taarifa za utabiri wa saa 24, siku 10, mwezi na tahadhari kama zinavyotolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA).*

## 2. MIFUMO YA HALI YA HEWA

Joto la Bahari la wastani hadi chini kidogo ya wastani linatarajiwa katika eneo la Tropiki ya Kati ya Bahari ya Pasifiki. Aidha, joto la Bahari la wastani linatarajiwa magharibi mwa Bahari ya Hindi (Pwani ya Afrika Mashariki) ikilinganishwa na joto la Bahari la juu kidogo ya wastani upande wa mashariki. Hali hii inatarajiwa kupunguza kasi ya msukumo wa hewa yenye unyevunyevu kutoka Bahari ya Hindi kuelekea maeneo ya ukanda wa pwani ya nchi yetu pamoja na maeneo ya jirani na hivyo kudhohofisha mifumo isababishayo mvua katika maeneo hayo.

Vilevile, joto la Bahari la wastani hadi juu kidogo ya wastani linatarajiwa katika eneo la pwani ya kusini mashariki mwa Bahari ya Atlantiki (Pwani ya Angola). Hali hii inatarajiwa kudhohofisha msukumo wa hewa yenye unyevunyevu kutoka misitu ya Kongo kuelekea maeneo ya magharibi mwa nchi na yale yaliyopo ukanda wa kati.

Kwa upande mwingine, joto la bahari katika eneo la kusini magharibi mwa Bahari ya Hindi (mashariki mwa kisiwa cha Madagascar) linatarajiwa kuwa juu kidogo ya wastani katika baadhi ya nyakati. Hali hii inatarajiwa kuchangia kutokea kwa migandamizo midogo ya hewa katika maeneo hayo, na kupelekea kuimarika kwa mifumo isababishayo mvua katika maeneo ya pwani ya kusini mwa nchi yetu, nyanda za juu za kusini magharibi na maeneo jirani.

## 3. ATHARI NA USHAURI

Athari na ushauri umeandaliwa na Mamlaka ya Hali ya Hewa kwa kushirikiana na wataalam wa sekta husika katika mkutano wa wadau wa hali ya hewa uliofanyika Dodoma tarehe 13 Oktoba, 2025.

### a) Kilimo na Usalama wa Chakula

Mvua za Chini ya Wastani zinazotarajiwa katika maeneo mengi zinaweza zikasababisha upungufu wa unyevu wa udongo, jambo ambalo linaweza kuathiri ukuaji na maendeleo ya mazao na kupunguza mavuno hususani kwa mazao yanayategemea mvua. Pia, kuna uwezekano wa kuongezeka kwa wadudu waharibifu wa mazao kama vile panya na mchwa.

Wakulima wanashauriwa kuandaa mashamba kwa wakati, kupanda, kupalilia na kutumia pembejeo husika kwa kuzingatia hali ya unyevu katika udongo. Aidha, wanashauriwa kutumia mbinu bora na teknolojia za kuhifadhi maji shambani. Vilevile, inashauriwa kuimarisha miundombinu ya kilimo na kudhibiti kwa wakati magonjwa ya mimea na wadudu waharibifu ili kupunguza madhara yanayoweza kujitokeza.

Wakulima wanashauriwa pia kutafuta taarifa sahihi kutoka kwa maafisa ugani kwa kuzingatia utabiri wa msimu wa wilaya husika katika kuchagua mbegu na zao sahihi. Aidha, wakulima na maafisa ugani wanashauriwa kuendelea kutumia utabiri wa siku na wa siku kumi ili kufuatilia kwa ukaribu mwenendo wa utabiri wa msimu.

### b) Mifugo na Uvuvi

Upungufu wa mvua unaotarajiwa katika maeneo mengi unaweza kuathiri upatikanaji wa maji na malisho kwa mifugo, hali ambayo inaweza kusababisha migogoro kati ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi.

Wafugaji wanashauriwa kuweka na kutekeleza mipango bora ya matumizi na uhifadhi wa maji pamoja na vyakula vya mifugo. Aidha, wafugaji na wavuvi wanashauriwa kutumia taarifa za utabiri wa hali ya hewa na kuzingatia ushauri unaotolewa na maofisa ugani ili kupunguza athari zinazoweza kujitokeza na kuendelea kunufaika na hali ya hewa inayotarajiwa wakati wa msimu.

*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*
Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Chuo Kikuu cha Dodoma,
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, 1 Mtaa wa CIVE,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610: Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz

### c) Utalii na Wanyamapori

Katika maeneo yanayotarajiwa kupata mvua za Chini ya Wastani, hifadhi za taifa na mapori ya akiba yanatarajiwa kukumbwa na upungufu wa malisho na maji kwa wanyamapori. Hali hii inaweza kusababisha migogoro kati ya wanyamapori na jamii zinazozunguka maeneo hayo. Wanyamapori wanaweza kuvamia makazi ya binadamu, hivyo kuongeza hatari ya maambukizi ya magonjwa kwa mifugo. Aidha, hali hii inaweza kuhatarisha usalama wa binadamu na wanyama wa kufugwa kutokana na mashambulizi ya wanyama wakali.

Mamlaka husika zinashauriwa kuboresha miundombinu mbalimbali katika mbuga na mapori ya akiba na kujenga uelewa kwa jamii ili kuchukua hatua stahiki kutokana na athari zinazoweza kujitokeza. Hivyo, jamii inashauriwa kutoa taarifa kwa mamlaka husika pindi wanyamapori wanapoingia katika maeneo yao ya makazi.

### d) Ujenzi, Usafiri na Usafirishaji

Sekta ya Usafiri na Usafirishaji inatarajiwa kunufaika kutokana na upungufu wa mvua katika msimu huu. Hata hivyo, uwezekano wa vipindi vifupi vya ongezeko la mvua vinaweza kuathiri au kusitisha shughuli kwa muda. Wadau wa sekta hii (usafirishaji nchi kavu, Majini na Angani) wanashauriwa kuchukua hatua stahiki katika utekelezaji wa ujenzi, ukarabati na matengenezo kinga ya miundombinu mbalimbali pamoja na ukaguzi wa mara kwa mara wa miundombinu ya usafiri na usafirishaji ili kupunguza au kuzuia madhara yanayoweza kujitokeza.

### e) Nishati, Maji na Madini

Kupungua kwa kina cha maji kwenye mabwawa na mtiririko wa maji kwenye mito kunaweza kutokea, hali ambayo inaweza kupunguza upatikanaji wa maji kwa matumizi mbalimbali na kusababisha migogoro kati ya watumiaji wakubwa na wadogo.

Uzalishaji wa umeme kwa kutumia nguvu za maji unaweza kuathiriwa. Hata hivyo, ujenzi wa miradi mipya ya uzalishaji umeme pamoja na utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi unaweza kunufaika na hali hii.

Katika sekta ya madini, uzalishaji wa madini kwa wachimbaji wadogo unaweza kuongezeka kutokana na upungufu wa mvua. Hata hivyo, shughuli za uchimbaji madini zinazotegemea maji kwa kiasi kikubwa zinaweza kuathirika.

Matumizi endelevu ya rasilimali maji na uvunaji wa maji ya mvua vinapendekezwa, hasa kwa ajili ya umwagiliaji, uzalishaji wa umeme wa maji, usindikaji wa madini, pamoja na matumizi ya viwandani na ya nyumbani. Aidha, jamii pamoja na mamlaka za maji na nishati zinashauriwa kuchukua tahadhari ili kulinda miundombinu na kupunguza athari zinazoweza kujitokeza.

*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*
Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Chuo Kikuu cha Dodoma,
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, 1 Mtaa wa CIVE,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610: Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz

**f) Mamlaka za Serikali za Mitaa**

Upungufu wa upatikanaji wa maji kwa matumizi ya nyumbani, kilimo, na mifugo unatarajiwa katika maeneo yanayotarajiwa kupata mvua Chini ya Wastani hadi Wastani. Hivyo, Mamlaka za Serikali za Mitaa zinashauriwa kuchukua hatua madhubuti ikiwemo kuimarisha na kuboresha mifumo ya usambazaji maji safi kwa matumizi ya nyumbani na Sekta nyingine muhimu. Hata hivyo, vipindi vya mvua kubwa katika baadhi ya maeneo vinaweza kusababisha kutuama kwa maji na mafuriko. Hali hii inaweza kusababisha uharibifu wa miundombinu na upotevu wa maisha na mali. Mamlaka za Serikali za Mitaa zinashauriwa kuboresha mifumo ya mifereji ya maji ili kupunguza athari zinazoweza kusababishwa na mafuriko sambamba na kutoa elimu kwa jamii juu ya hatua zinazopaswa kuchukuliwa katika utekelezaji wa shughuli za kijamii na kiuchumi

Vilevile, Mamlaka husika zinashauriwa kuongeza uelewa kwa Timu ya Usimamizi wa Halmashauri (CMT) kuhusu hali ya msimu unaotarajiwa na kuhamasisha uandaaji wa mipango na bajeti mahsusi kwa kila sekta ili kuongeza utayari na kupunguza athari zinazoweza kujitokeza. Hii ni pamoja na kuimarisha Kamati za Maafa kuanzia ngazi ya kijiji hadi wilaya ili kusimamia na kupunguza athari hizo.

**g) Sekta ya Afya**

Maeneo yanayotarajiwa kupata upungufu wa mvua, jamii inaweza kulazimika kutumia maji yasiyo safi na salama. Hivyo, mamlaka zinazohusika na afya ya umma pamoja na wananchi kwa ujumla wanashauriwa kuchukua tahadhari muhimu za kiafya ili kupunguza athari zinazoweza kujitokeza, kama vile kuhamasisha jamii kutibu maji kabla ya kuyatumia, kunywa maji safi na salama na kuhakikisha upatikanaji wa akiba ya kutosha ya dawa na vifaa tiba.

**h) Sekta Binafsi**

Shughuli za kilimobiashara na uzalishaji viwandani zinaweza kuathiriwa kutokana na upungufu wa mvua katika maeneo yanayopata msimu mmoja wa mvua kwa mwaka. Hali hii inaweza kusababisha ongezeko la gharama za upatikanaji wa malighafi na uendeshaji, pamoja na kuathiri ubora wa bidhaa kama vile miti ya nguzo, mbao, nyama na asali. Wadau wa Sekta Binafsi wanashauriwa kushirikiana na wataalamu mbalimbali, wakiwemo wataalamu wa hali ya hewa, ili kukabiliana na athari zinazoweza kujitokeza. Vilevile, taasisi za kifedha zikiwemo Benki, taasisi za Mikopo na Bima zinahimizwa kuandaa na kutoa huduma mahususi kwa wadau ili kujenga ustahimilivu na kuhakikisha uendelevu wa biashara.

**i) Usimamizi wa Maafa**

Hali ya upungufu wa mvua inayotarajiwa katika baadhi ya maeneo, hususan yanayotarajiwa kupata mvua za Chini ya Wastani hadi Wastani. Hali hii inaweza kusababisha upungufu wa maji safi na salama, kupungua kwa uzalishaji wa chakula na uhaba wa malisho kwa mifugo. Vilevile, vipindi vifupi vya mvua kubwa vinaweza kujitokeza na kusababisha mafuriko na maporomoko ya ardhi. Matukio haya yanaweza kuleta uharibifu wa miundombinu na mazingira, milipuko ya magonjwa, pamoja na upotevu wa mali na maisha. Idara ya Usimamizi wa Maafa, kwa kushirikiana na wadau mbalimbali nchini, inashauriwa kuendelea kuratibu na kutekeleza mipango ya kupunguza athari zinazoweza kujitokeza.

Aidha, Sekta mbalimbali pamoja na Kamati za Usimamizi wa Maafa katika ngazi za mkoa, wilaya, kata, na vijiji/mitaa zinashauriwa kuchukua hatua stahiki, ikiwa ni pamoja na kutoa elimu kuhusu usimamizi wa maafa na miongozo itakayosaidia katika kuzuia au kupunguza athari, kujiandaa na kukabiliana na maafa, pamoja na kuhamasisha uhifadhi wa chakula.

**j) Vyombo vya Habari**

Waandishi wa habari wanahimizwa kufuatilia na kupata kwa wakati taarifa za utabiri na tahadhari za hali ya hewa kutoka Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA). Hii itahakikisha utoaji wa taarifa kwa wakati ambazo zitasaidia kuelimisha umma kuhusu athari zinazoweza kusababishwa na hali ya hewa. Ni muhimu kusisitiza kuwa, kwa mujibu wa Sheria ya Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania Na. 2 ya mwaka 2019, ni kosa kisheria kusambaza taarifa za hali ya hewa kutoka vyanzo visivyo rasmi.

Aidha, wanahimizwa kushirikiana na wataalamu wa sekta husika ili kuandaa na kusambaza makala na ripoti za hali ya hewa kwa lugha nyepesi na inayoeleweka, zenye lengo la kusaidia jamii kuelewa na kutumia taarifa za utabiri wa hali ya hewa katika kupanga shughuli zao na kupunguza athari zinazoweza kusababishwa na mabadiliko ya hali ya hewa.

*Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania inawashauri watumiaji wa taarifa za hali ya hewa ikiwa ni pamoja na wakulima, wafugaji, Mamlaka za Wanyamapori, Mamlaka za Maji na Afya waendelee kutafuta, kupata na kuzingatia ushauri wa wataalamu katika sekta husika.*

*Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania itaendelea kufuatilia mwenendo wa mifumo ya hali ya hewa na kutoa mirejesho ya mwelekeo wa mvua nchini kadri inavyohitajika. Aidha, wadau wanashauriwa kuwasiliana na Mamlaka ili kupata taarifa mahsusi za utabiri wa msimu ili kukidhi mahitaji maalum katika sekta zao.*

**Imetolewa: 17 Oktoba, 2025**
**Na: Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania**